# KUTEKELEZA USHINDI WA KRISTO HADI DUNIANI

## Sehemu ya Kwanza

Na Jacquelyn Fedor
Ilitafsiriwa Na David Odhiambo

Mwanadamu alipewa mamlaka juu ya kila kitu ambacho Mungu aliumba duniani, yote yalikuwa yenye upatano na mema. Hakuridhika na mema, mwanadamu alitaka kujua ubaya kwa hiyo akachagua Mti wa Mema na Ubaya juu ya Mti wa Uzima. Wakawa matunda ya mti waliouchagua. Sasa wakimilikiwa naye, asili zao zilibadilishwa ili kuua, kuiba na kuharibu. Hapo awali walipenda kama Baba, kwa njia ya huruma na rehema. Upendo huu ulionyeshwa kwa viumbe vyote pamoja na kila mmoja wao, lakini macho yao yalifunguliwa kwa ulimwengu wa Shetani na sasa upendou ngechujwa kupitia tamaa ya jicho, tamaa ya mwili na kiburi cha uzima. Wangemiliki, sio upendo na sasa walikuwa tayari kwa mabadiliko zaidi.

Roho ya mwanadamu ilivunjwa na nafsi yake mwanadamu sasa alikuwa katika utumwa wa kuuridhisha mwili, ambao ulitawaliwa na Shetani. Kwa miaka 7,000 na zaidi na hii imekuwa hatima ya mwanadamu. Sisi leo tuko mbali na vizazi vingi kutoka kwa hali kamilifu tuliyokuwa hapo awali. Wakiwa wameshikwa mateka na Shetani na makundi mabaya yanayofuata mwelekeo wake, tamaa na matakwa ya hawa pepo wachafu yametoshelezwa kupitia sisi, vibaraka wao wa kibinadamu. Viumbe hawa waovu wamejifungamanisha kwa ukali na mwanadamu. Kiburi, hali duni, hasira,

woga, kumiliki, kudhibiti n.k. yote ni matunda ya pepo hawa wabaya wanaoongoza maisha yetu kupitia kamba za uovu ambazo sasa wanadamu wamezifunga katika kile ambacho kimekuwa nguo zake za kaburi.

Yesu aliweka mwanadamu huru, lakini bila kuelewa ni nini hasa alitimiza na kuelewa kikamilifu hitaji la wanadamu la ukombozi, mwanadamu bila kujua anaendelea kumtumikia bwana mbaya. Kwa hiyo mambo mawili yanahitajika sana, ujuzi wa kufahamu kikamili ukombozi wetu na wanadamu wapewe nafasi ya pili ili mwanadamu aweze kugeuzwa, kurejeshwa kwenye ukamilifu wake wa awali. Wokovu wa dunia na viumbe vyote hutegemea sana wale ambao Mungu aliwapa mamlaka ili kuwekwa huru. Wanawangoja watoto wa Mungu, kwa hivyo ni muhimu kwamba tutafute maarifa ya Mungu ambayo anarejesha kwa enzi hii.

**Warumi 8:19-21**

19 **Maana viumbe vyote** pia vinatazamia kwa shauku **kufunuliwa kwa wana wa Mungu**.

20 Kwa maana viumbe vyote vilitiishwa chini ya ubatili, si kwa kupenda kwake, bali kwa ajili yake yeye aliyevitiisha katika tumaini; (Ulimwengu wenyewe unateseka kutokana na dhambi na upotovu wa mwanadamu. Ni hali ya muda hata hivyo. Kuna tumaini la uhakika la ukombozi, lakini uhuru unategemea uchaguzi wa mwanadamu wa ujuzi na wake. kukubalika kwa mpango wa Mungu kwa njia ya Kristo.)

21 kwa sababu viumbe vyenyewe navyo vitakombolewa kutoka katika

utumwa wa uharibifu (au ugonjwa, kifo na uharibifu) hadi katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu.

Lakini, uhuru huu kamili hauwezekani, hata kama tunauona na kuuelewa, mpaka nguo za kaburi, kamba ambazo tumefunga kwa ulimwengu huu na nguvu za uovu zinazoidhibiti, ziondolewe. Lakini kwanza lazima tuone na kuamini yote ambayo Bwana alitimiza kupitia kutembea, kifo na ufufuo wake ili atuweke huru.

**Yohana 8:32** inaeleza hasa kwa nini ni lazima tuchague ujuzi wa Mungu uliotolewa kwa wakati huu.

32 Nanyi **mtaifahamu ukweli**, nayo hiyo **ukweli itawaweka huru**."

Hatuwezi kuisikia tu, lakini lazima tuijue na kuwa kitu kimoja ili kuwekwa huru Neno kujua katika Strongs ni 1097 maana yake: kutambua, kupata maarifa ambayo hayana mwanzo, maendeleo, kufikia kwa uzoefu wa ibinafsi.

**Waefeso 4:13** inaeleza Zaidi.

13 Mpaka sisi sote **tuje kwa umoja wa Imani** (wote wanasoma ufahamu wa wakati wa mwisho, iamini na utembee katika hiyo) na ya **ufahamu wa Mwana wa Mungu** (yote aliyatimiza), kwa **mtu kamili**, kwa **kipimo** cha urefu wa **Ukamilifu wa Kristo** (kwa hivyo mwili wake uweze kufanya kazi kwa nguvu na mamlaka yake);

Je! sisi, mwili wa Kristo, tunawezaje kuwaweka wanadamu huru hadi sisi wenyewe tuelewe Yubile kamili, au kazi kamili ya Mkombozi wetu? Neno linasema tunashinda kwa damu ya Mwanakondoo na kwa maneno ya ushuhuda wetu. Je! Tunawezaje kuhushudia na kushinda kesi yetu ikiwa tunakosa ukweli na bado tuko tunatembea kama ulimwengu?

**Waefeso 4:17-18**

17 Basi nasema haya, tena nashuhudia katika Bwana, kwamba msienende tena kama waenendavyo Mataifa wengine, katika **ubatili wa nia zao** (maarifa mabaya),

18 **akili zao zikiwa zimetiwa mbaya**, wametengwa na uzima wa Mungu (mtu alitengwa au kutengwa na nia ya Mungu kwa chaguo la Hawa), kwa sababu ya **ujinga wao wa kutojua**, kwa sababu ya **ukaidi wa mioyo yao**. (Matokea ya kuamini ujuzi wa Shetani juu ya Mungu);

**Waefeso 4:23-24** inatuongoza katika mwelekeo sahihi

23 na mfanye kufanywa wapya katika roho ya nia yako (kuanza kutembea kulingana na Neno),

24 na kwamba **mvae mtu mpya** aliyeumbwa **kulingana na Mungu**, katika haki ya kweli na utakatifu (kuzaliwa upya kwa njia ya Mungu kuwa kiumbe kipya).

**Yohane 3:3** Inatuonyesha nafasi hii ya pili.

3 Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakuambia, **Mtu asipozaliwa**

**mara ya pili,** hawezi kuuona **ufalme wa Mungu**.

Kuzaliwa upya ni zaidi ya wokovu. Kwa kweli humwezesha mwanadamu kustahili Ufalme wa Mungu, na kutufanya tustahili kuwa wale ambao Yeye atajenga ulimwengu Wake mpya na kusimamisha Ufalme Wake kupitia. Jamii mpya itazaa mifumo inayopatana na mapenzi ya Mungu kuchukua nafasi ya ile iliyopo sasa.

Changamka, kwa sababu kuna Yubile ya ulimwenguni pote au kuwekwa huru tunapoanza kujua ukweli.

Katika kujifunza neno Jubilee katika Strongs 8643 tunaona Yubile inawaweka huru wale wanaompenda Kristo na kuwarejesha wote waliopoteza kwa kosa la Adamu na Hawa. Pia, hata hivyo, itaharibu, kufuta, kuyeyusha wote wanaopinga watu wake na Ufalme wake.

Kwa hiyo **1 Wathesalonike 5:4-5** inatutia moyo kuwa na hakika sisi ni mmoja wa wale waliowekwa huru kutoka kwa ufalme wa giza na tumejitayarisha kuwa watoto wa Mungu waliorudishwa.
4 Lakini **nyinyi**, akina ndugu, **hamko gizani**, hata **siku hii iwapate**
kama mwizi.
5 **Nyinyi nyote ni wana wa nuru** na **wana wa mchana**. **Sisi** si **wa**
**usiku** wala **wa giza**.

Falme hizi mbili zinakabiliana kupitia wanadamu.

**Mathayo 13:37-43** ni mfano mzuri wa aina mbili tofauti za
watu wanaojaa falme hizo mbili.
37 Akajibu, akawaambia, "Apandaye zile mbegu njema ni Mwana wa
Adamu.
38 Shamba ni ulimwengu, **mbegu nzuri ni wana wa Ufalme** (Ufalme wa
Mungu), lakini **magugu ni wana wa yule** **mwovu** (au ufalme wa giza).
39 Adui aliyepanda ni Ibilisi, **mavuno ni mwisho wa nyakati**, na **wavunaji
ni malaika**.
40 Basi magugu zitakusanywa na huchomwa kwa moto; ndivyo
itakavyokuwa katika mwisho wa ulimwengu huu (wale watakaonyakuliwa
katika ulimwengu watakuwa na ishara za nje kuwa ni za Shetani).
41 **Mwana wa Adamu** **atawatuma malaika wake**, na **watakusanyika nje
ya ufalme wake vitu vyote vinavyokosea**, na **wale** ambao **hawana sharia**.
42 Na **atawatupa kwenye tunuru ya moto** (jubilee, kuwaweka huru dunia
na uumbaji wote) kutakuwa na kulia na kusaga meno.
43 Kisha **wenye haki watang'a kama jua katika ufalme wa Baba yao**.
Yeye ambaye ana masikio na asikie (watawekwa huru sio tu kutoka kwa
dhambi, lakini kwa upotovu na kwa adui)!

Kupitia Watoto wa Ufalme wa Giza na kupitia Watoto wa Ufalme wa Nuru, Vichwa viwili vya falme hizi vinapigana. Yesu ndiye kichwa cha mwili wake wa watu, Shetani ndiye kichwa juu ya mwili wake vile vile. Kwa mtazamo

wa kwanza watu wote wanaweza kuonekana sawa, lakini sio. Binadamu hata hivyo walianza kuwa kamili kama Baba.

**Mwanzo 1:27**
27 Kwa hiyo **Mungu akaumba mwanadamu kwa mfano wake mwenyewe**; kwa mfano wa Mungu alimuumba; wa **kiume na wa kike wote aliwaumba**.

**Mwanzo 3:1** mwanzo wa kuanguka kwa mwanadamu
1 Sasa **nyoka alikuwa mjanja Zaidi kuliko mnyama yeyote wa shamba** ambalo Bwana alikuwa ametengeneza. Akamwambia yule mwanamke, je! Mungu alisema, Hautakula kila mti wa bustani?

Alirudia kile ambacho Mungu alikuwa amesema, "usiguse, usionje", lakini kwa upumbavu alikula matunda ya akili ya Shetani, akipuuza mapenzi ya Mungu, mara nyingi Mungu anarejelea viumbe kama miti na anarejelea watu kama upandaji wa Bwana. Angalia Isaya 61:3.

**Ufunuo 20:1-2** inatuonyesha nyoka alikuwa nani.
1 Kisha nikaona malaika akishuka kutoka mbinguni, akiwa na ufunguo wa kuzimu na mnyororo mkubwa mkononi mwake.
2 Akamshika **yule joka**, **yule nyoka wa zamani**, ambaye **ni Ibilisi** na **Shetani**, akamfunga miaka elfu moja (haya yote ni majina yanayomrejelea adui, Shetani);

Yeye zaidi ya kitu chochote alichotaka na bado anataka kuwa kama Mungu.

**Isaya 14:14**

14 **Mimi** (shetani) nitapanda vilele vya mawingu **nita** jifanya **kuwa sawa na Mungu Mkuu**.

Katika jaribio la kuwa muumbaji aliyekubaliwa na mwanadamu, Mwanzo 6:12 inafunua kuvuka kwa watu pamoja na malaika, na kuzaa jamii iliyobadilishwa, ambayo Shetani ana haki kwao na anaweza kisheria kuwa kama vile Mungu wao.

**Mwanzo 6:1-2** inaleta mwangaza.

1 Binadamu walipozidi kuongezeka juu ya uso wa dunia, na kuzaa mabinti,
2 Kwamba wana wa Mungu (malaika) waliona mabinti wa wanadamu kuwa wazuri; **wakajitwalia wake** **wote** waliowachagua.

Henoko, wa 7 kutoka kwa Adamu, anafafanua zaidi.

**Henoko 15:3**

3 Kwa nini ninyi (Malaika) mmeiacha mbingu ya juu, takatifu na ya milele, **na kulala na wanawake**, na **kujitia unajisi** **kwa binti za wanadamu** na kujitwalia wenyewe wake, na **kufanya kama wana wa dunia**, na **kuzaa majitu** (kama) **wana** **wenyu**.

Hii lazima ilimkatisha Mungu tamaa, watu wake walijiruhusu kuvuka na spishi nyingine! Alielewa vizuri tatizo ambayo hili lingesababisha katika vizazi vijavyo. Watoto waliozaliwa na kasoro, Miili yetu haiwezi kuzuia magonjwa na udhaifu tena, tena na tena, kuvuka kwa spishi hii hii inaendelezwa na kupitia kwa mwanadamu kwa wito wa Shetani ili aweze kudai umiliki wa uumbaji wote, Wanyama, mimea nk. Tena, yote hay ani kwa sababu Shetani alitaka kuwa kama Mungu. Kwa kweli alibadilisha uumbaji ili aweze kuidai yake mwenyewe. Mungu kwa hasira aliwaangamiza wengi ya wanadamu kwa chukizo hii, lakini wakati huo huo alikuwa na mpango wa kumrejesha mwanadamu, ili amwachilie huru, kwa hiyo aliwahifadhi wanadamu wanane kwa huruma na jozi ya kila spishi aliyoiunda ka dunia.

**Mwanzo 6:6-7**

6 **Mwenzi Mungu alisikitika sana kwa kumuumba bindamu duniani**.
Mwenyezi Mungu alihuzunika sana moyoni mwake.
7 Basi Bwana akasema "**Nitamwangamiza mwanadamu ambaye mimemuumba** kutoka kwa uso wa dunia, mwanadamu na mnyama, kitu cha kutambaa na ndege wa angani, Ninasikitika sana kwamba niliwaumba duniani.

Nuhu alikuwa bado mwenye haki au angalau mwenye haki Zaidi kuliko wengi kwa hivyo Mungu alichagua kuendela na spishi za kibinadamu kupitia

yeye na wanawe.

**Mwanzo 6:18-19**

18 Lakini **nitaanzisha agano langu na wewe** (Noa); Nawe utaenda kwenye Safina **wewe**, **wana wako**, **mke wako**. Na **wake za wanawe**.

19 Nawe **utaingiza katika Safina jozi ya kila aina ya viumbe**, **wa kiume na wa kike**, ili **kuwahifadhi hai pamoja nawe**.

Ujumbe wa pembeni: wakati Mungu alikuwa anafanya agano na nuhu, alifanya ahadi na ulimwengu wote.

**Mwanzo 9:11**

11 Kwa hivyo **ninaanzisha agano langu na wewe**: Kamwe mwili wote hautakataliwa na maji ya mafuriko; **Kamwe** hakutakuwa na **mafuriko** ya **kuharibu dunia**.

Tuna upinde mbinguni kama ishara Mungu hatagharikisha dunia kwa maji ya kimwili tena lakini, kwa maji ya ukweli, maji ya uzima, oh ndiyo! Kwa kweli urejesho wetu unategemea mvua hii ya masika ya kiroho ili kutusaidia kukua katika  mwili uliokomaa wa Kristo. Ataifanya upya dunia na viumbe vyake vyote kupitia mafuriko haya ya maji ya uzima, ujuzi wake.

**Isaya 11:6-9** hufanya hili kuwa kweli!

6 "Mbwa mwitu pia atakaa na mwana-kondoo, chui atapumzika na mbuzi mchanga, ndama na mwanasimba watakula pamoja, na mtoto mdogo

atawaongoza.
7 Ng’ombe na dubu watakula pamoja, ndama wao watapumzika pamoja; na
simba atakula majani kama ng’ombe.
8 Mtoto mchanga atacheza kwenye shimo la nyoka, mtoto ataweza kuitia
mkono shimoni mwa nyoka mwenye sumu.
9 Katika mlima mtakatifu wa Mungu hakutakuwa na madhara wala uharibifu.
**Maana kumjua mwenyezi Munngu kutaenea pote nchini**, kama vile **maji inavyo funika bahari**.

Ukweli utatuweka huru kwani ufahamu wa Mungu utatiririka!

Kwa bahati mbaya damu ya malaika walioanguka bado ilikuwa sehemu ya ubinadamu kupitia Noa na wanawe. Kwa kweli tabia zao hupitishwa kizazi baada ya kizazi. Wale ambao hawajazaliwa tena bado wako katika hali hiiiliyobadilishwa leo. Shetani hataki wabadilishe hali yao kuwa kiumbe kipya kukombolewa au kuachiliwa huru na Bwana, angepoteza umiliki! Mwanadamu na yote waliobarikiwa nayo hapo awali wangerejeshwa wangerejeshwa kwa Baba na kuwa upande wake akarudi kwetu. Ukombozi wao, jubilee Shetani angelazimika kuwarudishia yote aliyopata kwa kumdanganya Hawa. Kuelewa kwa msimamo ubinadamu wote tayari umekombolewa na Bwana, lakini lazima tuione ichukue fursa hiyo. Wale ambao watamwamini wataingia paradiso ikiwa watakufa, kama mwizi msalabani lakini wale walio zaliwa kwa mara ya pili ambao huchagua maarifa ya Mung una huzaliwa kupitia Neno watakuwa wale ambao wana

sehemu ya kujenga mbingu na dunia mpya. Hawa spishi mpya, viumbe vipya vilivyozaliwa kupitia marifa ya Mungu, vitasababisha ushindi wa kristo Duniani!

Tembelea tovuti yetu http://www.trumpetsoftruth.com